CAMBRIDGE
International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **May/June 2024**

TRANSCRIPT **Approximately 45 minutes**

This document has **8** pages.

© Cambridge University Press & Assessment 2024



https://xtremepape.rs/

Eng: Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE Examination in Swahili
Paper 2, May/June 2024
Turn over now.

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: **Zoezi 1**

TLR: Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

TLR: Swali 1

M: * Leo niliaibika sana nilipofika dukani. Nilienda kununua vitu vingi sana na ilipofika wakati wa kulipa niligundua kwamba kadi yangu ya malipo haikuwa kwenye pochi kama nilivyotegemea. Halafu nilikumbuka kumwona mpwa wangu mdogo akicheza na pochi yangu, bila shaka kadi ilidondoka. Safari nyingine nitahakikisha kabla ya kutoka nyumbani. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 2

F: * Ninakuandikia ujumbe huu kukuhadithia mkasa ulionikumba juzi nilipokuwa Morogoro. Nilikuwa nimebeba mfuko wa mgongoni mzito ulionichosha hivyo nikaamua kuuweka juu ya jiwe lililokuwa karibu yangu ili nipumzike kidogo. Mara nyani aliruka kutoka mtini na kuunyakua mfuko wangu. Nilipiga ukelele lakini haikusaidia. Watu walicheka walipomwona ingawa mimi nilishtuka sana. Baada ya muda nyani aligundua mfuko wangu haukuwa na maana kwake akautupa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 3

M: * Mama baisikeli yangu ina pancha na lazima nitengeneze tairi leo ili kesho nisichelewe shule.

F: Sawa, bora fanya haraka.

M: Sina mpira na gundi ya kubandika kwenye tairi ili kulitengeneza na duka limeshafungwa.

F: Kwa nini hukusema tangu mwanzo? Sasa itabidi kesho nikupeleke shuleni kwa gari halafu ninunue mahitaji yako ili utengeneze baiskeli. Sikuwa na mpango wa kuendesha gari kesho.

M: Samahani mama, wakati mwingine nitapanda basi. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

TLR: Swali 4

F: * Nimenunua mmea wa kupanda ndani ya nyumba na kuumwagilia sana. Pia niliuweka dirishani ili upate jua lakini baada ya muda mfupi mmea wangu uligeuka rangi ya kahawia kabla ya kusinyaa. Nimelazimika kuutupa, jambo lililonisikitisha sana. Ninafikiri mara nyingine nitapunguza maji na nitafanya utafiti kabla ya kununua mmea wa ndani. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 5

M: * Kulikuwa na mashindano ya picha zinazoonyesha jiografia za sehemu tofauti duniani. Mimi nilipiga picha nyingi za vichochoro vyetu na niliamua kuingiza mojawapo kwenye mashindano. Nilipenda zaidi picha iliyokuwa na watu wakiuza kahawa barabarani na wengine wakinunua kahawa. Baada ya kufikiri kwa muda niliamua kuiingiza picha ambayo haikuwa na watu wowote kwani nilihisi iliakisi jiografia zaidi. Mwaka ujao kama kutakuwa na mashindano nitapeleka picha ambayo itakuwa na watu pia. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 6

M: * Ulianzaje kutengeneza ala ya muziki kama hii ya zeze?

F: Kusema kweli, binamu yangu alikuwa mwanamuziki aliyejulikana na siku moja tulienda kukiona kikundi chake kikicheza hapo kwenye jumba la maonyesho. Nilivutiwa na ala za muziki na baadaye, niliporudi nyumbani, ndipo nilipoanza kuwaza jinsi ya kuunda hizo ala. Tena si kwa kuzicheza lakini kwa kuwapa wanamuziki wazicheze na kufurahisha umati.

M: Safi sana. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 7

M: * Leo tufanye nini hapa Bagamoyo?

F: Twende kutazama magofu au jumba la makumbusho tulililoliona jana. Tutajifunza historia ya sehemu hii.

M: Kweli, ingawa bora kufanya hivyo na wazazi wetu. Labda twende kutembea baharini na kufurahia upepo mwanana pamoja na mchanga mzuri wa hapa?

F: Ninapenda wazo hilo sana; twende.

M: Lakini pia tunaweza kuzurura mjini na kuona wenyeji wanavyoishi?

F: Bora tuzurure siku nyingine. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

© Cambridge University Press & Assessment 2024


https://xtremepape.rs/

TLR: Swali 8

M * Karibu, ungependa kununua viatu gani?

F: Ninatafuta raba ili kuzivaa kwenye mashindano ya kukimbia.

M: Tunazo aina mbili. Je unavaa kiatu namba ngapi na pia ungependa rangi gani?

F: Ninavaa namba sita na sitaki viatu vyeupe wala vyeusi. Hizo rangi zilikuwa sare yetu ya shule na sasa sitaki kuzivaa maana nimezivaa miaka nenda miaka rudi.

M: Nitakuletea rangi zote tulizo nazo ili uamue.

F: Sawa, asante sana. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 2**

TLR: Utamsikia msichana anaongea kuhusu Kisiwa cha Tumbatu.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Tumbatu ni kisiwa cha tatu kwa ukubwa katika Visiwa vya Zanzibar vinavyopatikana Tanzania katika Afrika Mashariki. Kiko upande wa kaskazini-magharibi mwa mwambao wa kisiwa kikuu cha Zanzibar kinachoitwa Unguja. Kisiwa cha Tumbatu kina urefu wa kilomita 8 na upana wa kilomita 2 tu. Mabaharia huhofia miamba inayozunguka Tumbatu na kukitenga kwa kiasi fulani.

F: Kisiwa kina umuhimu wa kihistoria kwani Washirazi ambao inasemekana walifika Afrika ya Mashariki kwenye karne ya tisa kutoka Uajemi walifika hapo pia. Ilipofika karne ya kumi na mbili, kisiwa kilikuwa tayari kina wakazi wengi kiasi waliokuwa wakiishi hapo. Wakati huo makazi mengi ya Waswahili kwenye pwani ya Afrika Mashariki yalikuwa yakipanuka na kukua kutokana na watu kuhamia maeneo hayo. Habari nyingi za Tumbatu enzi hizo ziliandikwa kwenye Muswada wa Tumbatu ambao wataalamu waliuthamini kutokana na historia iliyoandikwa humo. Kwa bahati mbaya muswada huo uliungua kutokana na moto wa mwaka 1938 na hivi sasa hatunao tena.

F: Hivi sasa kisiwa kina wakazi wasiozidi 30,000 na hakuna usafiri wa chombo cha moto kama gari hapo kisiwani. Watu hutembea au hutumia baisikeli. Panapokuwa na mgonjwa au pale mjamzito anapotakiwa kusafirishwa, inabidi kumbeba kwenye machela. Serikali ya Zanzibar ilianza kujenga barabara moja zaidi ya miongo miwili iliyopita. Hadi leo haijamalizika na wenyeji wanahisi kisiwa kitakapojengeka, utamaduni wao utaharibiwa.

F: Uchumi wa Tumbatu unategemea kisiwa kikubwa cha Unguja. Katika miaka ya hivi karibuni umekuwa ukipanda na kushuka. Sekta inayotegemewa zaidi ni ile ya uvuvi ingawa utalii unaanza kukua kisiwani sasa. Watu wengi huja kutazama kisiwa na kufurahia kuona majengo yake ya kizamani na pia hupiga mbizi na kuchunguza bahari na maisha ya samaki.

© Cambridge University Press & Assessment 2024 

https://xtremepape.rs/

F: Kuna umuhimu wa kiuchumi kwa Tumbatu kufunguka zaidi kitalii. Watu wangependa kuona mazingira yake mazuri ya asili ambayo yana wanyamapori wadogo kama nyani. Kwa maoni yangu, kuna hatari kwa makazi ya wanyama kupotea kama utalii utakua kwa kasi sana. Hata hivyo sidhani kama kukuza utalii kutaharibu utamaduni. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 3**

TLR: Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu bustani zao.
Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha **A–G**.
Kwa kila msemaji, andika herufi (**A–G**) katika mstari wa jibu.
Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.
Utasikia rekodi mara mbili.

TLR: * Msimulizi 1

M: Nilijiunga na kundi la wakulima wa bustani za matunda na maua zilizopo mtaani kwangu takriban miezi miwili iliyopita. Sisi hukutana kila jumapili saa nne asubuhi na sijawahi kukosa hata mkutano mmoja. Nimekutana na jirani wengi na nimejifunza vitu vingi sana. Jambo nilipendalo zaidi ni pale tunapochuma matunda tuliyopanda na kugawana. Wiki hii tulichuma machenza mengi na nilipata bakuli zima. Hatuwezi kukutana bila kiongozi wetu kuwepo ingawa ningefurahi kama sera hii ingebadilishwa ili tupendezeshe mtaa zaidi na kupata matunda mengi. Kwa bahati mbaya yeye ana shughuli nyingi kwa hivyo si rahisi kumpata.

TLR: Msimulizi 2

F: Mtaani kwetu kuna kikundi cha wakulima wa bustani ambao hupalilia na kutengeneza vipande vya bustani vilivyo karibu na barabara. Sijui wanapata wapi muda wa kufanya hivyo. Tena wengi wao ni watu wazima ambao bila shaka wana ajira zao. Mimi bustani yangu mwenyewe tu inanishinda na imejaa magugu kwani sina nafasi ya kuishughulikia. Nikitoka kazini inabidi nipike, nijitayarishe kwa siku ya pili na nifanye kazi za ndani. Ningependa kukutana na jirani zangu lakini si kwa kulima, labda kama kungekuwa na kikundi cha kupika ningejiunga nacho.

TLR: Msimulizi 3

M: Siku hizi ukipita mtaani kwetu hutapatambua. Zamani kulikuwa na takataka, magugu yaliota kila sehemu na hakukuwa na maua mazuri. Unapotembea unakuta miwardi na miasumini iliyochipua na kumwagiliwa. Nilifurahia wazo langu la kuanzisha kikundi cha jirani cha kushughulikia maeneo ya bustani ambayo hayakuwa ya watu binafsi. Niliona kwamba ardhi ukingoni mwa barabara na pembeni ya sehemu ya kuegesha magari ilikuwa imekauka na haivutii. Watu wengi walifurahia wazo hilo na sasa tunapokutana tunasafisha, tunamwagilia na pia tunachuma matunda na kugawana. Pia tumejenga urafiki mzuri.



https://xtremepape.rs/

TLR: Msimulizi 4

F: Nilijiunga na kikundi cha wakulima wa bustani kijijini kwetu baada ya kugundua kuwa kuna watu wavivu hawapandi maua bali wananunua maua ya plastiki na kuyapachika ardhini. Maua hayo ya bandia hayapendezi asilani, hasa pale yanapopauka rangi. Sasa kundi letu limekuwa kubwa mno na hatuwezi kulima kwa starehe. Tena mimi hukereka sana kwani sioni tena raha ya kupalilia na kumwagilia kama hakuna nafasi ya kutosha. Mimi nina bustani binafsi iliyoshehena matunda hivyo sihitaji kuchukua ya mtaani ambayo hugawiwa baada ya kulima. Watu wengi huja kulima ili wapewe matunda ya bure na tena huleta watoto wao ili wacheze pale.

TLR: Msimulizi 5

M: Kikundi changu cha wapenzi wa mazingira ni kama familia yangu kabisa. Ninawafahamu watu wote pale kwani nimekuwa nikijishughulisha nao kwa muda mrefu sasa. Kusema kweli sipendi kazi za kupalilia na kutoa magugu; ninavutiwa zaidi na kumwagilia pale tunapotumia mfereji wa maji. Sipendi kabisa siku ambazo inabidi kumwagilia kwa kuchota maji na kuyajaza kwenye ndoo. Ingawa ninakereka kwa hili na lile lakini kamwe siwezi kuacha kujiunga na wenzangu. Wazo la kuchuma matunda na kugawana pia naliona kama la kipuuzi; ninahisi ingekuwa bora kama tungeuza matunda na kupata pesa kwa kikundi ili tujiendeleze.

TLR: Msimulizi 6

F: Siku hizi mtaani kwetu kumejaa familia zenye watoto wadogo kwa hivyo kundi letu la ukulima nalo limeathirika. Wao hukimbizana na kupiga kelele pale tunapokuwa tukihangaika na kazi. Zamani kundi lilijaa watu wazima na kulikuwa na utulivu zaidi. Nina hamu ya kuwaambia wazazi wasiwalete watoto wao kwenye shughuli zetu za kulima bustani lakini sitaki kuwakera. Mmoja alipachika maua ya plastiki kwenye bustani na wazazi hawakumgombeza. Kuna umuhimu wa kuwafanya wazazi wachukue zamu za kucheza na watoto kando ya bustani kama lazima wawepo. Kwa njia hiyo tutaweza kufanya kazi kwa ujirani mwema. **

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*

© Cambridge University Press & Assessment 2024 

https://xtremepape.rs/

TLR: **Zoezi 4**

TLR: Utasikia mazungumzo kati ya Aaliyah na Mikhail kuhusu mwandishi mashuhuri kutoka Zanzibar.
Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.
Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.
Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Juzi uliniambia kwamba mshindi wa Nobel ya fasihi ya mwaka 2021 ni mwafrika, hebu niambie unahisi vipi.

M: Yaani huu ni ushindi mkubwa mno kwani Abdulrazak ni mtu wa kwanza mwenye asili ya Afrika Mashariki kushinda tuzo hili. Atapata maelfu ya pesa za kigeni kuonyesha kuwa bara la Afrika lina waandishi waliobobea. Nilipopata habari ya heshima hii nilisherehekea mno kwa sababu yeye ni mmoja ya wachache wanaoandika kuhusu maisha ya watu wa Afrika Mashariki na hivyo anaakisi maisha yetu kabisa.

F: Alaa, anatumia lugha gani?

M: Lugha anayotumia ni Kiingereza ingawa riwaya zake huwa na maneno mengi ya Kiswahili. Yaani kama wewe ni mzaliwa wa Tanzania au Kenya utasikia raha sana. Watu wengi wanaona fahari ya asili yake katika matumizi yake ya lugha tofauti, lakini mimi ninadhani muhimu zaidi ni kwamba asili yake imemwezesha kuandika kiuhalisia kuhusu maisha ya Afrika Mashariki. Amefanikiwa kufanya hivi ingawa ameishi Uingereza kwa kitambo sasa.

F: Ungependa kama angaliandika kwa Kiswahili?

M: Unajua, ninahisi watu hupenda kuandika kwa kutumia lugha ambayo wanaitumia mara kwa mara wanapokuwa makwao. Hii huwa lugha inayowajia kirahisi zaidi na wanayoiheshimu. Kuna watu kama huyu Abdulrazak ambao wanaweza kuandika kwa lugha nyingi ila wanakuwa wamechagua kutumia mojawapo. Abdulrazak anazungumza Kiswahili fasaha, tena anazungumza vizuri kabisa lakini ninafikiri ni muhimu kuheshimu maamuzi yake.

F: Nimekuelewa. Yeye huandika kuhusu nini? Yaani mada yake kuu ni ipi?

M: Anaandika kuhusu mambo mengi sana. Ana riwaya ambazo zina mada za mapenzi na mahusiano ya watu. Pia huandika kuhusu mada za kisiasa kama ukoloni. Kwa kweli watu wanaopenda mambo tofauti wanapenda riwaya zake. Mada ambayo mimi ninahisi huwa kwenye vitabu vyake vyote ni ile ya kumbukumbu za kihistoria na ninadhani ni jambo hili linalowafanya wengi wavutiwe na kazi zake. Ningependa zaidi kama riwaya zake zisingeficha mada ya mapenzi.

F: Vijana wanapenda kweli mada hiyo. Je kuna eneo fulani ambalo kazi zake huakisi?

M: Kinachofurahisha kwenye riwaya zake ni kwamba kuna riwaya ambapo hataji majina ya maeneo ambapo hadithi hutokea. Hivyo huwaachia wasomaji waamue. Kuna hadithi moja ambayo mimi nina hakika inatokea miaka ya zamani jijini Dar es Salaam lakini mama yangu anadhani kwamba ni mji wa Pangani. Hii ndio hadithi yake inayonivutia zaidi kuliko zote kwani mwandishi amenipa nafasi kuamua hadithi inatokea wapi. Kuna hadithi nyingine ambapo yeye hutaja majina ya maeneo na watu wengine hupenda jambo hilo.

F: Niambie kuhusu ushindi wake, ilikuwaje?

M: Mimi niliona kwenye taarifa za habari kwamba washindi wa hizi tuzo huwa hawajui kabisa kama wanaweza kuchaguliwa hivyo wengi hushtuka sana wanaposhinda. Ingawa waandishi wengi wamepewa tuzo kwa ajili ya utaalamu wao wa kuandika, nilishangaa kuona mwandishi ambaye



https://xtremepape.rs/

hakujulikana sana alishinda. Hata hivyo, mimi kama shabiki mkubwa wa Abdulrazak ninahisi hii tuzo ilichelewa kumfikia.

F: Kwa hivyo hakuamini?

M: Ndio, hakuamini. Ninafikiri, kama wengi wanaofuatilia ratiba za tuzo za fasihi duniani, bila shaka mwandishi huyu alikuwa akisubiri kusikia nani angeshinda na nilisoma mahali kwamba alipopigiwa simu ili kupewa taarifa kwamba ni yeye aliyeshinda, yaani ni yeye atakayepata tuzo, alifikiri huyo aliyempigia simu alikuwa anamsanifu hivyo hakuamini. Tena nilisoma kwamba alihisi mtu alikuwa akimtania. Lakini bila shaka ilibidi aamini taarifa hii ilipoanza kusambaa kote duniani.

F: Nahisi ningependa kuwa mwandishi ili nishinde tuzo na kupata maelfu ya pesa.

M: Hata mimi ninahisi hivyo. Tena nimeanza kuandika hadithi. Siku hizi si vigumu kuchapisha vitabu na pia kuna mashindano mengi ya fasihi ambapo ninaweza kutuma hadithi zangu. Itabidi kushindana na watu waliokuwa wakiandika tangu utotoni ambao huandika vizuri sana.

F: Wewe andika, mengine utaangalia baadaye! **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

Eng: This is the end of the examination.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (Cambridge University Press & Assessment) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge International Education is the name of our awarding body and a part of Cambridge University Press & Assessment which is a department of the University of Cambridge.

© Cambridge University Press & Assessment 2024 

https://xtremepape.rs/